

## **Je! Yesu Atarudi Lini?**

**(Sehemu ya Pili)**

Juma lililopita tulianza somo kuhusa Yesu na atarudi lini. Leo tutamaliza somo kwa kufuata maandiko tu. Kwa sababu kama watu wa Mungu tunahitaji kuyaacha mafundisho ya uuongo. Na kama tunataka kujua ukweli katika kila jambo tunahitaji kurudi kwenye maandiko. Kwa hiyo leo tutaona: Jinsi Yesu atakaporudi na Kwa nini Yesu atakuja tena.

### **I. Yesu atarudi namna gani?**

- A. Watu wengine wanafundisha Yesu atarudi kwa siri. Kwa mfano Mashahidi ya Yehova walipanga siku ya kurudi kwake katika mwaka wa 1914 na baada ya hapo mwaka wa 1918. Lakini baada ya 1918 Mashahidi walianza kufundisha kwamba Yesu alikwisha rudi katika mwaka wa 1914. Lakini alionekana kwa watu wachachi tu. Lakini Biblia inatufundisha kwamba tusiamini kuwa Yesu atarudi kwa siri, Mat. 24:26. Na tukisoma mstari wa 27 tunaona kwamba Yesu atakuja kama radi na watu wote watamwona. Na tukiendelea na kusoma mistari ya 30-31 tunaona ya kuwa makabila yote, watu wote, wenye haki na wasio haki watamwona Yesu atakapokuja. Na Yohana anasema kwa ufupi na tena ni rahisi kuelewa katika Ufunuo 1:7, “Tazama, atakuja na mawingu, na kila jicho litamwona...”
- B. Yesu atarudi toka mbinguni na sauti ya malaika kuu pamoja na parapanda ya Mungu, 1 Thes. 4:16. Nyota za mbingu zitaanguka; na nguvu za dunia zitatemeka. Na atazungukwa na malaika zake na atakuja. Soma Mat. 24:29-31.
- C. Kwa hiyo Yesu atarudi na wakati wa kurudi kwake kila mtu atamwona, kila mtu atapiga magoti mbele wa Mungu na kukili ya kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu na kila mtu atajibu kuhusu maisha yake. Kwa hiyo Je! Yesu atarudi kwa siri au amekwisha rudi? La! Hasha!

### **II. Kwa nini Yesu atarudi tena?**

- A. Atapeleka ufalme kwa \_\_\_\_\_, 1 Kor. 15:24.
1. Kwa hiyo Yesu hatarudi kujenga ufalme wake, atarudi ili apeleke ufalme kwa Baba!
  2. Pia Paulo alisema Yesu anatakiwa kutawala kabla ya kuangamiza \_\_\_\_\_, 1 Kor. 15:25-26.
  3. Pia \_\_\_\_\_ itaagamiza wakati Yesu atafufua \_\_\_\_\_, 1 Kor. 15:52-57.
  4. Kwa hiyo Yesu anatakiwa kutawala kabla ya kurudi kwake mara ya pili sio baada kama madhehebu wanavyofundisha.
- B. Yesu atarudi ili afufue wafu.

1. Kumbuka kila mtu kama ni hai au amekwishakufa atamwona Yesu wakati atakaporudi, Ufu. 1:7.
  2. Saa inakuja wakati wale walio kwisha lala wasasikia \_\_\_\_\_ na wata \_\_\_\_\_, Yn. 5:28-29.
    - a. Watu wema watapata uzima wa \_\_\_\_\_.
    - b. Waovu wata \_\_\_\_\_.
  3. Paulo alisema wenye \_\_\_\_\_ na wasio na \_\_\_\_\_ wata \_\_\_\_\_, Mdo. 24:15.
    - a. Tuangalie yote hapa, Paulo alisema kutakuwa ufufuo wa wafu. Hakusema wenye haki na wasio haki watafuliwa wakati tofauti. Bali "Kutakuwa ufufuo wa wafu."
- C. Yesu atakuja kuhukumu watu wote.
1. Kila mtu \_\_\_\_\_ mwetu atatoa habari \_\_\_\_\_ zake \_\_\_\_\_ mbele wa \_\_\_\_\_, Rum. 14:12.
  2. Yesu atarudi ili kila mtu ajibu kuhusu matendo yake katika \_\_\_\_\_, 2 Kor. 5:10.
  3. Yesu atagawanya \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_, Mat. 25:31-32.
  4. Na waovu watatupwa \_\_\_\_\_, Mat. 25:41.
  5. Na kule motoni waovu \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_ meno, Mat. 25:30.
  6. Na moto ule ni wa milele kama mbinguni, 2 Thes. 1:9.

**Hitimisho:**

Yesu atarudi! Atawachukua watu wake waenda kukaa mbinguni. Kwa hiyo tuwe tayari kila saa. Kwa sababu tuna nyumba moja tu ya tumaini, na nyumba ile ni ya watakatifu kule mbinguni, 1 Pet. 1:3-4.